

Salaam hivi karibuni. (Picha na CCWV imakao imakuu).

HABARI LEO UK 20

*'Wafugaji wabadilike, wasomeshe watoto'

Na John Mhala, Monduli

MBUNGE wa Monduli mkoani Arusha, Fredy Lowassa amesema ili kuendana na kasi ya mabadi-liko ya teknolojia duniani na mabadi-liko ya tabianchi, jamii za kifugaji hazina budi kubadili mtizamo na kuwekeza katika elimu kwa watoto wao.

Fredy alisema hali ilivyo sasa, ni lazima jamii za wafugaji zikabadi-liko na kujikita zaidi katika elimu ya watoto wao na kuachana na dhana ya kuwa na idadi kubwa ya mifugo ambayo haiendeni na changamoto ya ardhi.

Alitoa wito huo wilayani Monduli wakati akitabidhi vifaa

mbalimbali vikiwemo magodoro, masanduku, madaftari, sare za shule na mahitaji mengine kwa wanafunzi zaidi ya 200 waliofaulu na kutakiwa kujiunga na kidato cha kwanza wilayani humo lakini wakashindwa kujiunga na kidato cha kwanza kwa kukosa vifaa.

"Tunashindana kuhusu mifugo, hakuna ujanja kwa sababu watu wanaongezeka, ardhi haiongezeki, ni kweli tumekuwa tukiamini kuwa mifugo ndiyo berki yetu lakini kwa hali ilivyo sasa haiwezekani," alisema.

Alisisitiza kuwa jamii ya wafugaji ya kifugaji inahitaji elimu zaidi kutohana na mfumo wa maisha yao.

Aidha, aliwataka wananchi wa Monduli kuenzi mawazo ya Waziri Mkuu Mstaafu, Edward Lowassa ambaye ni mwasisi wa shule za kata nchini kwa kuwatendea haki watoto wa jamii ya kimaasai kwenda shule.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Ole Sokoine, Thomas Lukumay alisema licha ya mwamko mkubwa wa elimu kwa wazazi, changamoto inayokabili wafugaji ni ukame kwani idadi kubwa ya mifugo imekufa.

"Karibia asilimia 35 ya wanafunzi waliopangiwa kujiunga kidato cha kwanza wameshindwa kuripoti shule kutohana na kukosa vifaa vya shule, wazazi wengi wanapiga simu kuomba muda wa

kuendelea kufanya maandalizi," alisema.

Baadhi ya wanafunzi waliopata msada huo, Mustapha Saimoni ambaye amepangienda kwenda Shule ya Sekondari Engutoto alisema alihuzuniaka alipoona wenzake wakienda shulen.

"Sasa mbunge anirudishia matumaini, nitaenda shule na ni-naahidi kusoma kwa bidi," alisema Mustapha.

Hafla hiyo ilihudhuriwa pia na viongozi wa mila (Laigwanani) ambao Freddy alishaomba wamsa-die kuhakikisha watoto waliofaulu wanakwenda shule bila kukosa, badala ya kuwaachia walimu peke yao ambao wana majukumu mengine.